**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

**8 MEI, 2023**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ i

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ ii

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1

1.0 **MAELEZO YA JUMLA** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Msingi wa Uchambuzi ........ 1

1.3 Mawanda ya Uchambuzi ........ 2

**SEHEMU YA PILI** ........ 3

2.0 **MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI** ........ 3

2.1 Ufafanuzi wa Jumla ........ 3

2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ........ 3

2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 4 ........ 3
2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05 ........ 5
2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ........ 6
2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida ........ 7
2.2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati ........ 9
2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi ........ 10

2.3.1 Makadirio ya Maduhuli ........ 10

2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida ........ 12

2.3.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ........ 14

**SEHEMU YA TATU** ........ 16

3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........ 16

3.1 Wizara ya Kilimo – Fungu 43 ........ 16
3.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05 ........ 20
3.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24 ........ 21
**SEHEMU YA NNE** ........ 22

4.0 **HITIMISHO** ........ 22

4.1 Maelezo ya Kuhitimisha ........ 22

4.2 Shukrani ........ 22

# ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Fungu 43 - Makadirio naMakusanyo Halisi katika mwaka wa fedha 2022/2023........................................................................................................4

**Jedwali Na. 2:** Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika Mwaka wa Fedha 2022/ 2023.......................................................................................... 5

**Jedwali Na. 3:** Fungu 43 Hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023..............7

**Jedwali Na. 4:** Fungu 05 Hali ya upatikanaji wa Fedha kwa Matumizi ya Kawaida ...8

**Jedwali Na. 5:** Fungu 43 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli..........................11

**Jedwali Na. 6:** Fungu 05 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli............ ..............11

**Jedwali Na. 7:** Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023...................................13

**Jedwali Na. 8**: Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023.................................... ....14

## SEHEMU YA KWANZA

# 1.0 MAELEZO YA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/ 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2022/2023 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne inahusu Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(1)(b) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Katika kutekeleza jukumu hili mnamo tarehe 28 - 30 Machi, 2023 Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa

Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Fungu 24-Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Kilimo kwa pamoja na Taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 43** ambalo ni Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** ambalo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika na, **Fungu 05** ambalo ni Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara ya kujiridhisha kuhusu hali halisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mafungu yaliyotajwa hapo juu.

## SEHEMU YA PILI

# 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

## 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa Kilimo. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo makuu mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2), baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili kuliwezesha Bunge kushauri ipasavyo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu yaani Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika – **Fungu 24** na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**.

Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kugharamia Miradi ya Maendeleo na Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Kilimo ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **Shilingi 5,017,732,000.00**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 3,284,264,647.71** sawa na **asilimia 65.5** ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01**

**Jedwali Na. 1: Fungu 43 - Makadirio naMakusanyo Halisi katika mwaka wa fedha 2022/2023**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| 5,017,732,000.00 | 3,284,264,647.71 | 65.5 |

**Chanzo: Randama ya bajeti ya 2022/2023 fungu 43**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba: -

**(a)** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara na Taasisi zake zilifikisha wastani wa **asilimia 65.5** ya lengo;

**(b)** Ukusanyaji huu pia unaweza kumaanisha kuwa makadirio ya maduhuli yalifanyika chini ya kiwango; na

**(c)** Mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

### 2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2022/2023, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **Shilingi 126,100,000,000**. Hadi kufikia mwezi Februarii, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 600,208,480** sawa na **asilimia 0.48** ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.02**

**Jedwali Na. 2: Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika Mwaka wa Fedha 2022/ 2023**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| 126,100,000,000 | 600,208,480 | 0.48 |

**Chanzo: Randama ya bajeti ya 2022/2023 Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo ya maduhuli kwa fungu 05 yanaonesha kwamba: -

(a) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefika **asilimia 0.48** tu ya lengo kwa kukusanya jumla ya **Shilingi 600,208,480** kati ya **Shilingi 126,100,000,000** zilizokusudiwa. Aidha, makusanyo haya hayaendani na matarajio na malengo ya Wizara.

(b) Kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa asilimia 75 ya muda wa utekelezaji umeshapita;

(c) Mwenendo huu wa makusanyo unaleta shaka kwenye makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli iwapo ulikuwa na uhalisia. Aidha, mwenendo huu wa makusanyo unaweza pia

kuashiria ukosefu wa mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa madhuhuli na usimamizi wake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo. Changamoto kubwa ipo kwenye ukusanyaji wa maduhuli ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo makusanyo yake hayaoneshi kufikia lengo.

### 2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo inatekeleza jumla ya miradi 41 chini ya Fungu 43, miradi 70 Fungu 05 na miradi miwili (2) Fungu 24. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharimia miradi hiyo ni **shilingi 631,506,114,000** sawa na **asilimia 84.07** ya bajeti ya Wizara ya Kilimo iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea Mradi Namba 4499 – **Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Nchini** (**TANIPAC**).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Maabara ya Utafiti kwenye Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Magonjwa ya Mimea Kibaha (National Biological Control Unit) ikiwa ni eneo mojawapo kati ya maeneo makuu matatu ya utekelezaji wa mradi wa TANIPAC. Kituo hiki kimepewa majukumu ya kutafiti na kusimamia (Research and Regulate) teknolojia mbalimbali za udhibiti wa magonjwa ya mimea kwa njia za kibaiolojia.

**Mhedhimiwa Spika,** thamani ya mradi huu ni **Shilingi 3,821,431,766.10.** Hadi Kamati inatembelea mradi huu, ulikuwa umekamilika kwa zaidi ya **asilimia 95** ambapo ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ukikamilika utalisaidia Taifa katika kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kudhibiti wadudu na magonjwa ya mimea kwa njia ya kibaiolojia, na kudhibiti usambaaji na madhara yatokanayo na sumukuvu. Kamati iliona kwamba, ili mradi huu ulete tija iliyokusudiwa wananchi hasa wakulima wapewe elimu kuhusu uwepo wa sumukuvu na matumizi sahihi ya viuatilifu kulingana na mazingira.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 99,655,547,000** sawa na **asilimia 38.7** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 43,124,232,629.65** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 54.7** ya bajeti iliyotengwa. Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa Mwaka 2022/2023.

**Jedwali Na. 3: Fungu 43 Hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 43 MWAKA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA.** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 49,403,470,000 | 32,100,446,625.82 | 65 |
| OC | 50,252,077,000 | 11,023,786,013.83 | 22 |
| **JUMLA** | **99,655,547,000** | **43,124,232,629.65** | **54.7** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 54.7** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) wa **asilimia 22** hairidhishi na hivyo kutoleta matumaini ya kukamilisha malengo yaliyokusudiwa hasa katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu – 05 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 5,268,352,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari, 2023, kiasi cha fedha kilichopokelewa ni **Shilingi 2,985,186,590.90** sawa na **asilimia 56.67** ya kiasi kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 04**.

**Jedwali Na. 4: Fungu 05 Hali ya upatikanaji wa Fedha kwa Matumizi ya Kawaida**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 05 MWAKA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA.** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 3,630,168,000 | 2,177,520,000.00 | 61 |
| OC | 1,638,184,000 | 807,666,390.00 | 49.2 |
| **JUMLA** | **5,268,352,000** | **2,985,186,590** | **56.7** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu - 05

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla ni **asilimia 56.7** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Mwenendo huu wa upatikaji wa fedha unaridhisha na kutoa mwelekeo wa ukamilishaji wa lengo lililokusudiwa. Aidha, lengo litakamilika ikiwa tu upatikanaji huu wa fedha utaenda sambamba na upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 14,693,267,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 93** ya bajeti ya Tume**.** Hadi kufikia Februari, 2023, Tume ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 9,248,574,145.50** sawa na **asilimia 62.9** ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida si mbaya na hivyo unaonesha kwamba utekelezaji wa lengo unaweza kufikiwa.

### 2.2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 43 Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilishauri mambo mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

**Mheshimiwa Spika** mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali imezingatia ushauri wa Kamati wa kuhakikisha fedha za maendeleo za ndani zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ambapo hadi kufikia Februari, 2023, Fungu 43 lilikuwa imepokea **asilimia 68** ya fedha za ndani zilizoidhinishwa;

(b) Serikali imepunguza makali ya upungufu wa watumishi katika sekta ya kilimo kwa kuajiri jumla ya watumishi 72 ambao ulikuwa ushauri wa Kamati.

Aidha, Kamati bado inasisitiza umuhimu wa Serikali kutenga bajeti ya kuajiri watumishi wa kutosha ili kuisaidia sekta hii kufikia malengo iliyojiwekea;

(c) Serikali imeandaa mpango wa utoaji ruzuku kwenye mbolea katika mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ambapo wakulima 2,936,737 wamesajiliwa kwenye mfumo kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku. Lengo likiwa ni kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji na kupunguza mfumuko wa bei ya vyakula; na

(d) Wizara kupitia TARI imejielekeza kwenye kukusanya na kusafisha mbegu za asili ambapo kwa mwaka 2022/2023 jumla ya mbegu za asili 84 (55 za mpunga, 14 za mtama, 12 za mahindi na 3 za uwele) zimekusanywa na kusafishwa. Zoezi hili ni endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua mbalimbali, Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

## 2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi

### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi 6,677,254,000**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 34** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.5** hapa chini.

**Jedwali Na. 5: Fungu 43 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| CHANZO | 2022/2023 | 2023/2024 | Nyongeza/ Pungufu% | Nyongeza/ Pungufu% |
| | 5,017,732,000.00 | 6,677,254,000 | 1,659,522,000 | 34 |

**Chanzo: Randama ya Wizara Fungu -43**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yameongezeka kwa **asilimia 34** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kufikia **asilimia 66** ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, Kamati inaona uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

(c) **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 05 -** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 10,000,000,000** ambayo ni pungufu kwa **asilimia 92** ya lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **Jedwali Na. 6** kinaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na. 6: Fungu 05 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| CHANZO | 2022/2023 | 2023/2024 | Nyongeza/ Pungufu% | Nyongeza/ Pungufu% |
| Mfuko (NIDF) | 126,100,000,000 | 10,000,000,000 | (116,100,000,000) | -92 |

**Chanzo: Randama Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2023/2024 yameshuka kwa **asilimia 92** ikilinganishwa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Pamoja na makadirio ya maduhuli kupungua kwa **asilimia 92** yakilishangishwa na mwaka 2022/2023, Kamati haioni namna ambavyo Tume inaweza kufikia lengo kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambao ulifikia **asilimia 0.48** tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji ikiwa mikakati ya ukusanyaji na vyanzo ni vilevile vilivyotumika katika mwaka unaoisha.

(c) **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati inaona kuwa ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, makadirio ya makusanyo yazingatie uhalisia ili utekelezaji wake uwe rahisi.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia **Shilingi 199,363,030,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa **asilimia 66.5** ikilinganishwa na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa katika bajeti ya Wizara ya Kilimo kuna ongezeko la **asilimia 66.5** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 07.**

**Jedwali Na. 7: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Na. | FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 99,655,547,000.00 | 109,319,631,000 | 9 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 5,268,352,000.00 | 73,547,775,000 | 1,288 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 15,793,267,000 | 17,383,074,000 | 10 |
| | | **JUMLA** | **120,717,166,000.00** | **200,250,480,000** | **66** |

***Chanzo*: Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ongezeko la **asilimia 66** kwenye bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati inaona kuwa huu ni mwelekeo mzuri kwani fedha hizi zitaongeza msukumo wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji bajeti ya miradi ya maendeleo. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe fedha hizi zinatolewa kwa wakati na kwa kadiri ya mahitaji ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Aidha**, ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida linatoa mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa programu za kilimo cha umwagiliaji hususan kuimarisha mifumo ya makusanyo ya mapato ya mfuko wa umwagiliaji pamoja na kujenga na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji hasa katika Programu ya *Building a Better Tomorrow* (BBT). Programu hii inatarajiwa kuchangia mpango wa Serikali wa kutengeneza ajira zipatazo **milioni tatu** kupitia kilimo nchini ifikapo mwaka 2025. Hatua hizi zinaakisi Ibara ya 37 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambayo imeahidi kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya Kilimo na mazingira sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko hilo la bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati inaona kiasi kilichoongezwa hakikidhi mahitaji kulingana na uzito wa majukumu makubwa yaliyopo katika kuhakikisha tija inaongezeka kwenye kilimo kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 767,835,139,000** kwa ajili ya kugharimia miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Makadirio hayo ni ongezeko la **asilimia 5** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 08**.

**Jedwali Na. 8: Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| NA. | FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 370,306,114,000 | 465,698,366,000 | 26 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 257,500,000,000 | 299,964,223,000 | 16 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 1,100,000,000 | 2,172,550,000 | 109 |
| | | **JUMLA** | **731,161,661,000** | **767,835,139,000** | **5** |

***Chanzo: Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba: -

a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeongezeka kwa **asilimia 5** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023;

b) Pamoja na bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo kuongezeka kwa **asilimia 5**, ongezeko hili bado halijakidhi mahitaji ya Wizara ambayo ni **Shilingi Trilioni 2** kwa mwaka;

c) Kiasi cha fedha zilizotengwa kutekeleza Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ya bajeti ya Taifa bado haijakidhi matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) ambalo linazitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo; na

d) Nyongeza ya bajeti ya maendeleo ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa **asilimia 109** inatoa mwelekeo mzuri wa Tume katika kuendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuimarisha Vyama vya Ushirika na kuviwezesha kujiendesha kibiashara;

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huu ni wazi kuwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake zitaongeza uwezo wa utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ni maoni ya Kamati kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unaweza kuwa na mafanikio endapo Wizara itapewa fedha zilizoombwa kwa wakati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ninaomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 3.1 Wizara ya Kilimo – Fungu 43

a) Pamoja na Serikali kuendelea kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo, bado haikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) ambalo linazitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga bajeti na fedha hizo kutolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa kufanyika kwa wakati;

b) Mfumo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea unalenga kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na hivyo kupunguza mfumuko wa bei za mazao. Hata hivyo, mfumo huu bado haujafahamika kwa wakulima wengi na hivyo kutoleta tija iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali: -

i) Kuhakikisha kuwa elimu na taarifa ya uwepo wa mbolea ya ruzuku na namna ya kuipata inatolewa ili kudhibiti mianya inayotumiwa na watu wachache ya kuuza mbolea kwa bei ambayo ni nje ya bei ya ruzuku;

ii) Wizara ipanue wigo na kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora na sahihi ya mbolea pamoja na viuatilifu; na

iii) Wizara iratibu na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbolea na viuatilifu unazingatia muda sahihi wa kilimo ili kuongeza tija iliyokusudiwa;

c) Hakuna tija katika kilimo bila uwepo wa wataalam (maafisa ugani) ambapo mahitaji ni takribani wagani 20,000, lakini waliopo 7,000 tu sawa na **asilimia 35** ya mahitaji. Upungufu huu hauwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga bajeti na kuajiri maafisa ugani wa kutosha pamoja na kuendelea kuimarisha matumizi ya kidijitali katika kutoa huduma za ugani ili ile tija iliyokusudiwa kwenye kilimo ipatikane;

d) Mazao ya kimkakati bado hayajawekewa mazingira rafiki ya kuhakikisha yanaendelea kuwepo na kukua kutokana na kukosekana kwa soko la uhakika. Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha soko la uhakika la ndani na nje ya nchi linapatikana wakati wote ili tija ya uwekezaji katika kilimo ipatikane. Aidha, mazao haya yawekewe mnyororo wa thamani hapa nchini ili kuhakikisha mkulima ananufaika;

e) Hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvuna bado iko kwenye tarakimu mbili (**asilimia 35**) ukilinganisha na shabaha ya kupunguza upotevu huo hadi **asilimia 5** ifikapo mwaka 2030. Hali hii inaweza kuathiri usalama wa chakula ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa chakula cha uhakika wakati wote nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi chakula kwa kukamilisha ujenzi wa maghala katika ngazi za vijiji, Kata na Wilaya hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula ili kuimarisha usalama na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna;

f) Programu ya Kujenga Kesho Bora (BBT) ambayo imelenga kuinua uchumi wa vijana na wanawake wa Tanzania kupitia kilimo ni hatua nzuri kwa Taifa. Aidha, ili kuleta tija inayokusudiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

i) Serikali iweke mfumo mzuri wa kuhakikisha programu hii inakuwa endelevu na kuendelea kuzalisha ajira kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa;

ii) Serikali ianzishe programu hii katika kanda zote nchini

iii) Serikali ihakikishe kuwa programu inachukua maeneo mengi yenye vyanzo vya maji ili kupunguza gharama za kujenga miundombinu ya umwagiliaji;

iv) Zoezi la umilikishaji ardhi lifanyike kwa umakini mkubwa;

v) Serikali ihakikishe upatikanaji wa masoko ya bidhaa zitakazozalishwa ni wa uhakika na unazingatia mnyororo wa thamani; na

vi) Serikali iweke mikakati ambayo vijana wanaopata ujuzi kupitia programu hii wataweza kutumika kusambaza ujuzi huo ili uendelee kunufaisha vijana wengine na jamii kwa ujumla.

g) Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 26.1 ya pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda, na mazao ya kilimo yamechangia takribani Dola za Marekani Bilioni 1.2 ya mauzo nje ya nchi. Kwa umuhimu huo Kamati inaishauri Serikali kuanzisha somo la kilimo kama somo la lazima kuanzia ngazi ya msingi ili kuwajengea vijana wa Kitanzania uwezo wa

kukielewa na kushiriki kikamilifu katika sekta na kuongeza ajira.

h) Mahitaji ya mbegu bora na za kutosha ni suala ambalo haliepukiki iwapo tunataka kuzalisha kwa tija na kuwanufaisha wakulima na wananchi kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuziwezesha taasisi zinazohusika na uzalishaji wa mbegu kifedha pamoja na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji ili ziweze kuzalisha kuzalisha mbegu bora na kutosheleza mahitaji yaliyopo nchini. Aidha, nguvu zaidi za uzalishaji wa mazao mahsusi, zielekezwe katika maeneo ambayo mazao hayo yanastawi kwa wingi ili kupata uzalishaji bora na wenye tija badala ya kuanzisha maeneo ambayo ni ya majaribio;

i) Maendeleo ya sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inahitaji kuziwezesha taasisi zake za utafiti ili kuongeza tija katika kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali: -

   i) Kuendelea kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa ajili ya utafiti na kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini;

   ii) Kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za asili (mbegu za Wakulima) kwa kufanyiwa utafiti, kuzalishwa kwa wingi ili kukidhi mahitaji na kuendelea kuboreshwa. Uzalishaji na utumiaji wa mbegu za asili utachangia katika kulinda utamaduni wetu, kuhakikisha uwepo wa usalama wa vyakula pamoja na kuinua kipato cha mkulima na uchumi wa Taifa kwa ujumla; na

iii) Matokeo ya tafiti zinazofanywa na taasisi zetu yawafikie na kuwasaidia wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija na kuongeza kipato.

### 3.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Utekelezaji wa Mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Ukusanyaji hafifu wa mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji unaipotezea Serikali mapato. Kamati inashauri Tume kuandaa mkakati wa kuimarisha mifumo ya makusanyo ya mapato ya Mfuko wa Umwagiliaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa hasa baada ya kuongezewa fedha za OC kwa **asilimia 1,288;**

Ili kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, Kamati inashauri ujenzi wa skimu mpya za umwagiliaji uzingatie maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, ili miradi hiyo iwe endelevu ni vyema ikashirikisha Serikali za Wilaya pamoja na Halmashauri husika; na

b) Serikali imejiwekea malengo ya kufikisha eneo la umwagiliaji hekta milioni nane (8) ambayo ni sawa na hekta milioni moja (1) kwa mwaka. Mpango wa kuwainua wakulima na kukiinua kilimo cha Tanzania ili kufikia lengo la kukuza sekta ya Kilimo kwa 10% ambayo imepewa jina la Ajenda 10/30, unaonesha mwelekeo mzuri wa kutoka katika kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara ifikapo 2030. Kamati inapongeza jitihada hizi na kuishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha kila mwaka

kwa uwiano utakaowezesha utekelezaji wa mpango huu kufikia lengo lililokusudiwa

**3.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24**

a) Kukosekana kwa wataalam wa kutosha katika sekta ya Ushirika, kumesababisha maendeleo ya Ushirika nchini kukosa tija iliyokusudiwa. Kamati inashauri Serikali kuajiri wataalam wa ushirika wa kutosha ili waweze kuendesha ushirika kwa uadilifu na tija iliyokusudiwa ipatikane;

b) Ili mchango wa Ushirika katika mageuzi ya kiuchumi upatikane, lazima chombo kinachohusika katika usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika kiimarishwe. Kamati inaishauri Serikali kuliongezea nguvu Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ili liweze kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ufuatiliaji na ukaguzi ambayo itapelekea kuimarika kwa utawala bora katika vyama vya ushirika;

c) Pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Benki ya Ushirika, bado Benki hii inakabiliwa na upungufu wa mtaji wa kutosha jambo linaloweza kupunguza tija. Kamati inaishauri Serikali: -

(i) Kuendelea kuimarisha benki hii kwa kuhakikisha inapata mtaji toshelevu;

(ii) Iweke mfumo mzuri utakaoviwezesha vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na Vyama vingine vya Ushirika nchini kununua Hisa za Benki hii kama njia ya kuimarisha na kukuza mtaji; na

(iii) Benki isogeze huduma karibu na wananchi kwa kufungua matawi katika mikoa mingi nchini.

**SEHEMU YA NNE**

# 4.0 HITIMISHO

## 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** Maendeleo katika Sekta ya Kilimo ni muhimu hasa katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hii una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote. Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 29.1 ya pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda, na mazao ya kilimo yamechangia takriban Dola za Marekani Bilioni 1.2 ya mauzo nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa Mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia (SGDs) hususani lengo namba 1 linalohusu kupunguza umaskini uliokithiri na lengo namba 2 linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

## 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano waliounesha kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina lakini naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb- Mjumbe
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb, - Mjumbe
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb- Mjumbe
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Prof. Patrick Aloysi Ndakimeki, - Mjumbe
18. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Yahya Ally Khamis, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood. Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha

uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Hussein Bashe (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. Anthony Mavunde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Mweli, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu Bwana Hussein Mohamed Omary.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndg. Athuman Hussein, *ndc,* Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* – Kaimu Mkurugenzi Kamati za Bunge, Makatibu wa Kamati ; Ndg. Elieka Saanya, Ndg. Thuwaiba Jumbe na Ndg. Asia Msangi na Ndg. Mwimbe John kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43, 24 na Fungu 05), kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

8 Mei, 2023